

# Ave Maria

Comp: Wachira Sammy

St Gregory choir Vol. 1

Malindi

Ma ma ye tu Ma ri a kwe li u me ba ri ki wa si si wa na o ma ma le o

tu na ku sa li mu li mu A ve a ve a ve Ma ri a sa la mu sa la mu Ma

ri a Bi ki ra Ma ri a kwe li u me ba ri ki wa A ve ki wa

1. Nyo ta ya 'su bu hi che m che mi ya fu ra ha Ma ma wa ke Mu ngu mwe  
U li ye ki ngi wa - - dha mbi ya a si li tu o mbe Ma ma kwa

...  
...

nye ba ra ka te le na o  
ke Ye su mwa

1. 2.

...

**Mama yetu Maria kweli umebarikiwa sisi wanao mama leo tunakusalimu X2**  
**Ave ave ave Maria salamu Maria (Bikira Maria) kweliumebarikiwa X2**

1. a) Nyota ya asubuhi chemchemi ya furaha, mama wake Mungu mwenye Baraka tele  
 b) Uliyekingwa dhambi ya asili, tuombee mama kwake Yesu mwanaao
2. a) Chombo cha heshima mwenye moyo safi, msaada wetu tunakukimbilia  
 b) Mama mtimilifu nyumba ya dhahabu, unatupatanisha naye Yesu mwanaao
3. a) Mlango wa mbingu na afya ya wagonjwa, mwenye huruma tele utuombee mama  
 b) Uliyepalizwa kwa Mungu juu mbinguni, utuongoze mama tufikie mbinguni
4. a) Waridi la moyo moyo ulio safi, msaada wa wanyonge twakulilia mama  
 b) Pendo la ajabu kuzaa mkombozi, dunia nzima sasa tunakushangilia